KWAYA YA MTAKATIFU KIZITO
PAROKIA YA MWENYEHERI ANUARITE MAKUBURI
+255742000089|+255713975788
kmkmakuburi
www.kmkmakuburi.co.tz
stkizitochoir@gmail.com

MWOKOZI WANGU UNISHIBISHE-KIPENDI

Kiitikio

Mwokozi wangu unishibeshe, kwa chakula chako chenye uzima.
Mwokozi wangu unishibeshe, kwa kinywaji chako chenye uzima.
Najongea meza yako nipokee, unisamehe dhambi na kunipa neema (bwana) kwa chakula chako chenye uzima wa milele.
Najongea meza yako nipokee, unisamehe dhambi na kunipa neema (bwana) kwa kinywaji chako chenye uzima wa milele

Mashairi

1. Ee Yesu, mwokozi, uliyekufaa msalabani ukaniondolea dhambi na mauti, unipokee

2. Ee Yesu, mwokozi, karibu moyoni mwangu sasa ukae ndani yangu nami ndani yako, nifarijike

3. Kwa mwili, na damu, nipate neema za milele ili siku moja nifike Mbinguni, kwenye uzima